


**Wafanyakazi wa Kampuni ya Mitiki Ofisi ya Dar Es Salaam**

**Kutoka kushoto Kulia Khadija, Francis, Barnabas, Fambo na Arlene**

**SIKILIZA KIPINDI CHA REDIO "MITIKI YETU" PAMBAZUKO 89.5 FM KILA IJUMAA SAA 1:30-2:00 JIONI & JUMAMOSI 1:30-2:00 ASUBUHI**

**KVTC ILIANZISHWA 1992**

# Kutoka Dawati la Irvine

KVTC imekusudia kuboresha uwiano wa jinsia katika nyadhifa mbalimbali na msingi wa kandarasi wake.
Kila mwaka tunaongeza jitihada kuhakikisha kampuni inatoa taswira ya uwiano wa jamii inayofanya nayo kazi.
Katika mda wa miaka 5 kampuni imeweza kuongeza mara dufu asilimia ya wanawake waajiliwa kufikia 27%.
Miaka 5 nyuma kampuni haikuwa na Afisa Misitu mwana mke lakini sasa inayo afisa misitu 5 waliobobea.
Kiasi cha 70% ya hodhi ya kampuni inahifadhiwa. Kampuni imejitahidi kulitunza bila kuharibiwa kupitia program mbalimbali za uhifadhi na ulinzi.

Kampuni inaenda hatua zaidi kuhakikisha kwamba maeneo Hifadhi ya thamani hadhimu natambuliwa katika tafiti iliofanywa mwaka jana yanalindwa na hadhi yake inaimarishwa.
Program zote hizi zinaweza kuendelezwa tu Kwa kuhakikisha KVTC inaendelea kuwa na faida. Utawala utahakikisha inaendelea kuwa hivyo sasa na mbeleni

## Kwa Heri KVTC.

**Na Hanta Rwegoshora**

Nilijiunga na TANWAT moja ya kampuni za CDC Tanzania January 1990. Wakati huu sikuwa na ndoto ya kufanya kazi KVTC kwa kuwa kampuni hii haikuwepo. Ilikuwa 1992 ndipo CDC iliunda kampuni ya KVTC na kuipa majukumu TANWAT kusimamia na kuangalia hatua za awali za uanzishaji wa KVTC. Wakati huu CDC ilifungua office ya mawasiliano Dar Es Salaam (DPSO) kuzipa huduma za usaidizi wa muungano wa makampuni ya CDC Tanzania. Hizi zilijumuisha TANWAT, EUTCO, Kibena Tea, Wakulima Tea na baadae KVTC. Nilijikuta nafanya kazi KVTC wakati inaanzishwa. Nilipewa jukumu la kutoa huduma za usaidizi ambao inajumuisha kununua bidhaa za mtaji na vitendea kazi kama vifaa vya mashambani, mashine za viwandani, mbegu za mitiki na miche / mapandikizi na zaidi ya vifaa vinavyohusiana na mahitaji ya ofisi

Mwaka 2008 KVTC ilibadilika kutoka mradi wa msitu au shamba. Na kuwa mradi kamili wa kampuni ya misitu jumuishi ikiwa pamoja na kiwanda cha kisasa cha kuchakata mazao ya mtiki kwa mauzo ya ndani na nje. Uongozi mpya uliundwa na majukumu ya DPSO yalibadilika na kuwa office ya kuunganisha inayo hudumia KVTC peke yake.

Kwa utaratibu mpya, majukumu yangu yalibadilika na kujumuisha kuwezesha / usaidizi shughuli za kuuza nje.

Shukrani kwa umakini wa uongozi KVTC kutekeleza kanuni, kampuni ilipata imani kwa wadau wote. Imani ilisaidia kupata wateja na wafanya biashara wa kuaminika. Hii ilisaidia kupunguza gharama zisizo husiana na uzalishaji ambazo zingeongeza mzigo katika mnyololo mzima.

Mapema 2023, Nilianza kujiandaa kustaafu kwa kumfundisha Fambo Etamagwe kama mrithi wangu.

Mwisho wa 2023, mrithi wangu tayari ana udhibiti mzuri kwenye nafasi hii. Sija simamisha kutoa msaada unao hitajika kuhakikisha uendeleve wa shughuli za KVTC. Rasmi nilistaafu January 1, 2024. Hata hivyo Naendelea kutoa huduma za ushauri kama na wakati ikihitajika.

Kitu pekee katika historia yangu, nilishiriki wakati kampuni inaanzishwa, ukuaji wake na ninaondoka katika hatua ikiendelea kuwa kampuni kubwa kabisa endelevu ya mitiki Afrika. Ya kutiwa mfano Afrika kwenye misitu dhaminifu.

Kuna mambo ya msingi nilio jifunza kwa maisha ya kufanya kazi KVTC

1. Kujitetea kwa kushindwa kutoa matokeo hakuongezi thamani katika utendaji wa kazi
2. Kuna njia mbadala wakati wote wa kutatua matatizo, tafiti fursa zote zilizopo kabla hujakata tamaa au kuomba msaada
3. Mafanikio yanapatikana kwa kushirikiana, kufanya kazi kwa bidii, uadirifu, uvumilivu na kumwamini upendo wa Mungu

Kitu nitakacho kikosa KVTC ni marafiki wa kweli, timu ya wabobezi na wachapa kazi na simu mbalimbali zinazo hitaji msaada.



Hanta Rwegoshora

## Ofisi ya KVTC Dar Es Salaam

**Na Arlene Gomes**

Ofisi ya KVTC Dar es Salaam inatoa huduma za usaidizi kwenye shughuli za msingi za Kampuni ya Mitiki katika Bonde la Kilombero. Timu imetengenezwa na wafanyakazi wawili wa kike na watatu wa kiume, wote ni watanzania. Timu inatekeleza shughuli zote za manunuzi na shughuli zote za kuuza nje za kampuni.

Khadija Bakari aliajiriwa Oktoba 2009 na alifanya kazi kama kalani msaidizi Mavimba, Ifakara. Oktoba 2013 alihamishiwa ofisi ya Dar Es Salaam na kufanya kazi kama kalani wa utawala. Majukumu yake ni kutekeleza majukumu ya utawala katika ofisi. Anapokea hati za madai (Invoice) zote kutoka kwa wagavi na kuhakikisha ziko sawa kabla ya kuziwakilisha kwenye kitengo cha uhasibu.

Francis Kimonje aliajiriwa Machi 2008 na anafanya kazi kama kalani wa mauzo ya nje. Majukumu yake ni kufuatilia na kupata vibali vya vya kuuza nje mbao za mitiki inayo safirishwa India na masoko ya nje.

Barnabas Mkude ameajiriwa Machi 2008 na anafanya kazi kama kalani wa mauzo ya nje. Majukumu yake ni kutuma maombi kwa vibali vyote vya mauzo ya nje kwa tekehama, Pamoja na shughuli nyingine.

Fambo Etamagwe aliajiriwa Mei 2011 na alifanya kazi makao makuu Kijiji cha Mavimba kama mhasibu na msimamizi wa store, aliajiriwa Mei 2011 mpaka Novemba 2023. Desemba 2023 alihamishwa Dar Es Salaam kwa kupandishwa cheo kama Afisa Manunuzi.Anahusika na manunuzi ya vifaa / mali ghafi ndani na nje ya nchi.

Arlene Gomes aliajiriwa Novemba 2017 na ni Meneja Biashara wa Kampuni.

Jukumu lake ni kusimamia taratibu za kubuku makontena, magari ya mizigo, kunyanyua mizigo kutoka kiwandani, kupeleka Dar Es Salaam na maandalizi ya nyaraka zote zinazo hitajika kwa usafirishaji nje. Arlene vilevile ana wajibu wa kuwakilisha nyaraka zote za usafirishaji mzigo kwa meli katika benki za wateja ambazo zina anzisha hatua za malipo. Arlene ana mchango mkubwa katika majukumu ya kampuni kiutawala na kibenki.

## Maria Mrema

**Na Maria Mrema**



Habari, Mimi ni Maria Mrema. Nimeolewa nina mtoto mmoja. Nilijiunga na KVTC 2022 nafanya kazi kama Meneja wa Eneo la Magogo "Log Yard manager". KVTC ina eneo kiini la magogo ambalo linapokea magogo yote kutoka msituni. Magogo yanashushwa, pimwa, yanalinganishwa na kupangwa kulingana na saizi na ubora. Timu ya wafanyakazi wa eneo la magogo ina wajibika kugawa magogo kwa wanunuzi 6 wa nje wa magogo na kiwanda cha kampuni.

Timu yangu ina msimamizi 1, waendesha machine ya kupakia magogo wa 4, na wafanyakazi wa kuhesabu 8, nne kati ya hao ni wanawake.

Uhitaji wa mda mrefu wamaisha yangu ni kutembelea maeneo ya misitu. Ilinipelekea kusoma digrii ya sayansi ya Misitu Chuo kikuu cha kilimo. (SUA). Nili hitimu 2019.

Kuanzia 2019 hadi 2021 nilipata elimu ya vitendo Mamlaka ya Huduma ya Misitu Tanzania (TFSA) ambako nilifanya kazi kama Afisa wa Eneo. Niliongoza wafanyakazi wachache katika kuokota mbegu. Elimu ya vitendo na uzoefu niliopata kutokana na elimu ya vitendo chuo kikuu ilinipa ujasiri wa kujiunga na KVTC.

Napenda kuhamasisha ushirikiano na kufanya kazi kama timu mmoja, wakati wote tukijitahidi kupata vipimo sahihi kufikia malengo ya kampuni na kufanya kazi kwa umakini.

Lengo langu ni kuhakikisha majukumu ya eneo la magogo lina simamiwa vizuri kwa mafanikio ya kampuni.

## Mafunzo ya Hifadhi ya thamani hadhimu KVTC

**Na Joseph John**

KVTC inasimamia eneo la hekta 28,132 ya ardhi. Kiasi cha 30% imepandwa mitiki na 70% imetengwa kwa malengo ya hifadhi. Eneo la hifadhi la KVTC (20,000ha) lina mchango muhimu katika eneo hilo na linaweza kuwa ushoruba wa wanyama pori kati ya hifadhi ya milima ya Udzungwa na Hifadhi ya Nyerere. Vilevile ni makimbilio ya Wanyama na vile vile ni eneo lenye thamani ya juu ya binuwai.

January 2023, maeneo ya asili ya yalitathminiwa kutambua hadhi madaraja ya Hifadhi ya thamani hadhimu (HCVA). Tafiti ilifanywa na wataalamu kutoka kampuni ya washauri kutoka taasisi ya uvyetishaji Misitu Mazingira (EFC). na ilihusisha majadiliano na wadau mbalimbali, upimaji shirikishi na utambuzi pori (HCVA) na kuziunganisha na jiografia kwa kupitia mfumo wa Taarifa za jiografia kwa kompyuta (GIS).

Tafiti ilithibitisha ardhi ya KVTC ina madaraja yote sita ya HCVAs. Tafiti ilishauri mikakati mbalimbali na programu ya ufuatiliaji kulinda hizi (HCVAs) ambayo itaboresha uwepo viumbe adimu, vinavyotishiwa na hatarini kutoweka na vilevile kutoa hifadhi wa wanyama pori kutoka katika maeneo yasiyo hifadhiwa.

Februari 2024, Uongozi wa KVTC uli andaa mafunzo juu ya Hifadhi ya thamani hadhimu (HCVAs). Mafunzo yalifanyika Ifakara mjini katika ukumbi wa Taasisi ya afya Ifakara. Iliwezeshwa na EFC wataalamu walewale waliofanya tafiti. Jumla ya watu 63 walipata mafunzo, Hii ilijumuisha wawakilishi wa wakandarasi wa Misitu, Askari wa mazingira wa vijiji (VGS), Meneja wa mashamba ya Kupandwa, Meneja Misitu, Jamii, Afya na Usalama kazini



Dr Richard Giliba (EFC) Akitiririka kwa ufasaha.

Mafunzo yalifanyika Februari 19 na 20, 2024, na ilikuwa na lengo kujenga uelewa mzuri wa umuhimu wa HCV na kuwajenga uwezo jinsi ya kutunza HCVAs bila zenyewa kuathiriwa na shughuli yeyote ya misitu.
Mafunzo ya siku mbili yalifanikiwa kupata malengo yafuatayo.

- Washiriki walipata kuelimishwa athari za ukataji miti na mabadiliko ya tabia nchi katika eneo lao, kitaifa na kiulimwengu.
- Washiriki walipata kuelimishwa juu ya dhana na madaraja ya HCVAs ukitegemea juu ya mwongozo wa HCVNR na sehemu halisi ziliko kwenye ramani
- Washiriki walipata kuelimishwa namna ya kusimamia maeneo ya HCV aidha kuyatunza au kuyaimarisha hadhi yake.
- Washiriki walipata kuelimishwa juu ya kuyafuatilia hadhi ya HCVAs zilizotambuliwa.
- Washiriki waliweza kutambua matishio na jinsi a kuzidhibiti vitishio tofauti ambayo inaweza kuwa na madhara kwenye HCVAs

Mafunzo haya yalisaidia washiriki kuboresha maarifa yao na ujuzi kwenye dhana ya HCVAs na kubadilishana uzoefu juu ya changamoto mbalimbali ya kuhifadhi. Haya mabadiliko yatakuwa na athari chanya kwenye jitihada za kuhifadhi na ahadi ya kulinda makundi yote ya HCVAs kwa kushirikiana na wadau wote wa eneo husika na kitaifa kwa manufaa ya mazingira, utamaduni na kijamii



Mpaka kati ya Ardhi ya KVTC na Kijiji cha Mbasa

.

## Ziara ya Viongozi wa KVTC Kwenye Mashamba ya Misitu

**Na Geofrey Kessy**

Julai 12, 2023, wafanyakazi wa idara ya misitu waliandaa ziara kwa meneja wote wanaofanya kazi makao makuu Mavimba. Lengo la ziara ni kuwapa uelewa mzuri nini wafanyakazi wa idara ya misitu wanakabiriana kila siku katika Maisha yao ya kazi.

Ziara ili zingatia mzunguko mzima wa mnyololo wa ongezeko la thamani katika msitu kuanzia shughuli za bustani hadi uvunaji na usafirishaji.

1. **Programu ya Uzalishaji na uboreshaji bustani ya KVTC**

Wafanyakazi wa bustani wakiongozwa na Jeremiah Gumadi na Cleria Kahemela walikuwa na fursa wakuonyesha uzalishaji miche na miche vipande (*stumps*). KVTC inabadilisha kutoka kutumika miche vipande kutumia miche iliyoboreshwa (*Clones*). Cleria alipata fursa kuelezea kile alichojifunza Costa Rica juu ya kuzalisha *clonal* za mtiki.

Jeremiah alielezea program ya uboreshaji wa miundo mbinu ambapo kampuni inawekeza katika ujenzi wa nyumba nyingine maalumu ya kukuzia mimea (*greenhouses*).

2. **Shughuli za ukuzaji Miti**

Meneja wa Mashamba la Miti, Yusta Abel, Godi Mwampamba and Gudrun Barnabas walipata fursa ya kuonyesha shughuli zao kuanzia kuandaa shamba lililovunwa hadi upandaji na usimamizi wa mitiki mpaka uvunaji. Walizingatia mada zifuatazo upaliliaji, kupogeleal matawi, kuweka mbolea na ulinzi wa moto.

3. **Tafiti na Mipango**

Kitengo cha Mipango Pamoja na majukumu mengine inawajibika katika kutathmini aseti za biolojia kwenye kampuni. Ikiongozwa na Yusuph Kihwele na Emanuel Manuma, walionyesha kwa meneja waliowatembelea jinsi wanavyofanya tathmini ambayo ni muhimu katika shughuli ya kupanga na kuthamanisha biashara nzima. Jeremiah Gumadi vilevile alipata fursa kuelezea moja ya tafiti katika shamba C ambako programu ya uboreshaji wa vina saba unaendelea.

4. **Uvunaji na Usafirishaji**

Amidu Karim and Hezron Revocatus wanahusika na uvunaji wa mitiki, yote mbili uvunaji na upunguziaji na usafirishaji wa magogo kiwandani



Amidu Karim na Hezron Revocatus na sehemu ya wafanyakazi (Waliosimama)

Wanawajibika vilevile na kusimamia utunzaji Barabara za msituni.

Katika shamba D99 shamba D, Amidu na wafanyakazi wenzake walionyesha kwa uongozi jinsi gani wanatekeleza shughuli zao za kila siku.

1. **Uboreshaji wa Kambi ya Misitu**

KVTC inaboresha makazi ya meneja wa mashamaba ya miti na wafanyakazi wa kupambana na moto. Programu ilianza 2021 ambapo makazi ya Mafinji shamba D yaliboreshwa na kukamilika 2022. Meneja Mkuu wa Shamba Geofrey Kessy alielezea jinsi gani kitengo chake ilivyopangilia kuboresha kambi za mashambani ikijumuisha kuunganisha nyumba na umeme wa taifa au kuweka umeme wa jua.



Kambi ya Nakafulu inayoboreshwa kwa Picha iliyopigwa na Drone

Ziara kama hii inafikiriwa kwa wawakilishi wa chama cha wafanyakazi